KWA NINI MASHIA HUSUJUDU JUU YA UDONGO?

Kimeandikwa na
Allama Sheikh Abdulhusain Al-Amini

Kimetafsiriwa na
Sayyid Muhammad Mahdi Al-Muusawy Shushtary

Kimetolewa na
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033,
DAR ES SALAAM, TANZANIA.

KWA NINI MASHIA HUSUJUDU JUU YA UDONGO?

Kimeandikwa na:

Allama Sheikh Abdul Hussain al-Amini

Kimetafsiriwa na
Sayyid Muhammad Mahdi al-Musawy Shushtary

Kimetolewa na Kimechapishwa na
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033
Dar es Salaam - Tanzania

Haki za kunakili imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania

ISBN 9976 956 52 5

Toleo ya Kwanza:	1979	Nakala:	2,000
Toleo ya Pili:	1990	Nakala:	2,500

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA
S.L.P 20033
DAR ES SALAAM - TANZANIA

YALIYOMO

1. Dibaji 1
2. Utangulizi 3
3. Kusujudu na vitu vinavyoruhusiwa kusujudia 6
4. Hadithi zithibitishazo kuwa ni wajibu kusujudu katika Ardhi .8
5. Hadithi zinazoruhusu kusujudu katika vitu vinginevyo 14
6. Hadithi zinazoruhusu kusujudu katika vitu vinginevyo kwa udhuru fulani 19
7. Uamuzi wa Haki 26
8. Kusujudu katika Udongo wa Karbala 28

DIBAJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye Kuneemesha, Mwenye Kurehemu

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa shukrani nyingi kwa kunipa uwezo wa kuendeleza matamanio yangu ya kufasiri na kuandika vitabu vya kidini kwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha ndugu zetu wa Kiafrika kupata maarifa zaidi ya dini ya ya Kiislamu kwa kupitia Madhehebu ya Ahlul-Bait wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) ijulikanayo kwa Jina la "Shia Ithna-ashari."

Baada ya kutunga kitabu "Mambo Yanayomhusu Maiti", nimeona ni afadhali na fardhi kwangu kujishughulisha na masuala yanayowakera Waislamu wengi wasiojua miongoni mwa ndugu zetu wa Kisunni; ambayo bila sababu ya maana na msingi wowote huleta tuhuma, chuki na utengano kati ya Waislamu.

Moja katika masuala hayo yanayoulizwa na ndugu zetu ni, "Kwa nini Mashia husujudu juu ya udongo?" Kusita kwao kutafiti jibu lake katika vitabu vyao wenyewe kunawafanya watutuhumu sisi eti kwamba tunavisujudia na kuviabudu vipande vya udongo!!!

Kijitabu hiki ni tafsiri ya sehemu moja ya kitabu kiitwacho

سيرتنا وسنتناسيرة نبينا (صلى الله عليه وآله وسلم) وسنته

(Mienendo Yetu na Sunna Zetu ni Mienendo ya Mtume Wetu (s.a.w.w) na Sunna Zake) kilichoandikwa na mwanachuoni mashuhuri wa Kishia, Hayati Allamah Sheikh Abdul-Hussain Al-Amini. Mtungaji huyu ameandika vitabu vingi vyenye kutoa majibu ya masuala yanayowatatiza ndugu zetu wa Kisunni. Kimoja katika vitabu vyake vilivyo maarufu ni kile kinachoitwa *Al-Ghadir*.

Katika kitabu hiki, Allamah Al-Amini hakuacha kunukuu japo hadithi moja kutoka katika vitabu maarufu vya wanavyuoni mashuhuri wa Kisunni yenye kuthibitisha jambo hili.

Mtungaji amezigawa hadithi hizo katika mafungu matatu. Sehemu ya kwanza ni zile Hadithi zenye kuonyesha kwamba ni lazima kusujudu katika ardhi unaposujudu katika sala. Suhumu ya pili ni ni zile Hadithi zinazoruhusu kusujudu juu ya vitu vingine badala ya ardhi (kwa mfano mkeka) bila ya udhuru wowote na Sehemu ya tatu ni zile Hadithi zinazomruhusu mwenye udhuru kusujudu juu ya vitu vingine badala ya ardhi.

Mwishowe, Allama Amini amethibitisha ubora na umuhimu wa kusujudu juu ya udongo mkatifu wa Karbala kwa sababu ya kuhusika na Mwenyezi Mungu.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu kwa baraka ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Ahlul-Bait (a.s.) wake atupe Taufiki ya kutuwezesha kuendelea kuwaelezea ndugu zetu sunna halisi za Mtukufu Mtume (s.a.w.).

Sayyid Muhammad Mahdi al-Musawy

Tehran, Iran
11th July, 1977.

UTANGULIZI

Sala ni tawi la kwanza na muhimu kabisa la vitendo vya dini ya Kiislamu, kwani "huzuia mambo ya aibu na maovu",[1] "ni njia ya kuombea msaada,"[2] "ni faradhi iliyowekewa nyakati,"[3] na "ni moja katika mafanikio ya walioamini",[4] na kadhalika.

Hayo yote ni kwa sababu sala, kama alivyosema Mtukufu Mtume (s.a.w.), "Ni nguzo ya dini. Ikikubaliwa, vitendo yyote hukubaliwa pia, na ikiktaliwa vitendo vyote navyo hukataliwa."

Kwa hivyo, ili kuhakikisha kwamba sala zetu zinakubaliwa, itatubidi tutekeleze masharti yote yanayohusu taratibu sahihi za sala, kwa mfano, kutamka maneno ya sala barabara, kusimama, kurukuu na kusujudu kama inavvotakikana. Masharti haya yanapofuatwa kikamilifu, sala yako huwa barabara. Lakini hayo hayatoshi kwa kutakabaliwa kwa sala yako, lwani hayo ni katika taratibu ya sala yenyewe tu.

Kuna masharti mengine yanayotangulia sala ambayo humbidi kila Mwislamu ayazingatie ili sala yake iwe sahihi. Baadhi ya masharti yenyewe ni haya:-

Kwanza, ni lazima mwili na mavazi yako yawe nadhifu, tohara na ya halali, na mahali unaposali pawe hivyo hivyo pia; pili, ni lazima utawadhe kwa utaratibu unaotakiwa, n.k.

1 Mwenyezi Mungu Anasema, "..... Bila shaka Sala huzuia mambo ya aibu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu ni (jambo) kubwa kabisa..." (Qur'ani, 29:45).

2 Mwenyezi Mungu anasema, "Enyi mlioamini, ombeni msaada kwa subira na Sala;..." (Qur'ani, 2:153).

3 Mwenyezi Mungu anasema, "..... Kwa hakika Sala kwa walioamini ni faradhi iliyowekewa nyakati." (Qur'ani, 4:103).

4 Mwenyezi Mungu anasema, "Hakika wamefaulu waaminio. Ambao katika Sala zao ni wanyenyekevu." (Qur'ani, 23:1-2)

Masharti haya na mengine yanafahamiwa vema na Waislamu wote, isipokuwa sharti moja muhimu ambalo ndugu zetu Masunni wanajaribu kulipuuza, nalo ni faradhi ya kusujudu juu ya ardhi au udongo; kwani hairuhusiwi kwa mwenye kusali kusujudia vitu vingine badala ya ardhi au vitu visivyoliwa au kuvaliwa vitokavyo humo ardhini bila ya udhuru wowote.

Kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba sala yako ni sahihi na inakubaliwa ni lazima unaposali usujudu juu ya ardhi (udongo) au kitu kiotacho au kitokacho humo ambacho hakiliwi wala hakivaliwi; kwa mfano, kipande cha udongo, kijiwe, busati, jamvi, mkeka na kadhalika.

Ikiwa utasujudu katika vitu vingine visivyokuwa hivyo, mathalan, msala uliofumwa kwa pamba au hariri, basi hapana shaka yoyote kwamba sala yako haitasihi, maadamu huna udhuru wowote. Kwa nini? Kwa sababu ni kinyume cha sunna na maamrisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na ni kinyume cha masharti ya sala.

Hadithi nyingi na zilizo sahihi zimepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) zisemazo kwamba Mwenyezi Mungu amejaalia ardhi kuwa ni tohara na mahali pa kusujudia. Na Mtume mwenyewe alikuwa akisujudu katika udongo, kijiwe au khumra (mkeka), wala hakuna hadithi sahihi hata moja inayoonyesha kwamba Mtume (s.a.w.w) aliruhusu au alikuwa akisujudu katika zulia, msala usiofumwa kwa majani au katika mavazi yake bila ya udhuru wowote.

Kinyume chake Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliwaamrisha masahaba wake wasujudu katika udongo, vijiwe au mkeka na aliwaamrisha kabisa wasisujudu katika vilemba vyao (ambavyo ni katika vitu vinavyovaliwa).

Kwa kuifuata amri na sunna hiyo, masahaba walikuwa wakipoza

vijiwe vilivyokuwa moto (kwa ajili ya jua kali) ili waweze kusujudu juu yao, kwa kuwa walijua kwamba kwa kutofanya hivyo sala zao hazitasihi.

Naam, ingawa ardhi imefanywa mahali pa kusujudia, lakini tunajua kwamba sio kuwa unaweza kusujudu kila mahali kwa sababu mahali unaposujudia lazima pawe tohara. Vile vile, tunajua kwamba ni vigumu sana kuhakikisha utohara wa mahali wanapokusanyika watu, kama barabarani, hotelini, vituo vya mabasi, reli n.k., kwa kuwa mahali hapo huwepo kila aina ya watu, Waislamu na wasio Waislamu, ambao hawajali maamrisho ya dini kuhusu tohara na najisi. Jambo hili huwa tatizo kubwa hususan kwa msafiri.

Hivyo, ili kujiepusha na tatizo hilo, kuna kipingamizi gani ikiwa Mwislamu (mwenye kuzingatia usahihi wa sala yake) atatumia kipande cha udongo ambao ataweza kusujudia anapokuwa safarini au mahali pasipo tohara?

Ikiwa ataamua kutumia udongo wa kusujudia, bila shaka atachagua udongo mtakatifu kabisa wenye sifa za kipekee ambao umehusika sana na Mwenyezi Mungu. Je, udongo huo ni upi?

Hapana shaka udongo huo ni wa ardhi ya Karbala. Udongo ambao ulilowa kwa damu ya Imamu Husain (a.s.) pamoja na Waislamu watiifu ambao walizitoa mhanga roho zao na kumwaga damu yao ili kuiokoa Dini Tukufu ya Mwenyezi Mungu - ISLAMU; udongo ambao kama usingelikuwa bora kabisa, Mwenyezi Mungu asingewatuma malaika wake kwa Mtume Muhammad (s.a.w.w) kumpelekea udongo huo na kumpasha habari ya kuuawa kwa mjukuu wake.

Kwa nini Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alinusa udongo huo na kulia? Kwa nini aliubusu na kuuweka kuwa ukumbusho? Kwa sababu

ulikuwa udongo ambao juu yake ingemwagika damu ya wana wa Mashahidi, Mpenzi wake na Mpenzi wa Mola wake, Bwana wa Vijana wa Peponi, Imamu wa Waislamu, Mwokozi wa dini ya Islamu kwa damu yake, ambaye kwa sifa hizo amepata uhusiano ulio karibu kabisa na Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu na Mtume wake wameutukuza udongo wa Karbala namna hiyo sembuse sisi tunaodai kufuata sunna zao? Ikiwa tunajua kwamba moja katika masharti ya sala ni kusujudu katika ardhi, basi kwa nini tusisujudu katika udongo mtakatifu wa ardhi ya Karbala? Kitu gani kinachokufanya usujudu katika zulia, msala wa pamba au hariri au nguo ambapo wajua kwamba sala yako haikubaliwi kama paji lako la uso haligusi ardhi?

Hadithi na hoja zilizotolewa humu zatosha kujibu swali, "Kwa nini Mashia Husujudu katika Udongo?"

KUSUJUDU NA VITU VINAVYORUHUSIWA KUSUJUDIA

Moja katika wajibu wa mwenye kusali ni kusujudu juu ya ardhi na kuifanya kuwa ni mahali pa kusujudia. Waislamu wote wanaafikiana kwamba mwenye kusali lazima asujudu juu ya ardhi. Katika hadithi sahihi, Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema:

جُعِلَتْ لِيَ الْأَرْضُ مَسْجِداً وَطَهُوْراً

"Mwenyezi Mungu amenifanyia ardhi kuwa mahali pa kusujudia na tohara."

Maimamu wa madhehebu zote za Kiislamu wanaafikiana kwamba inapoyumkinika ni lazima mtu asujudu juu ya ardhi au juu ya vitu vinavyoota katika ardhi. Tutanakili baadaye hadithi zenye kusadikisha maneno haya.

Hapo awali, Masahaba wa Mtume (s.a.w.w) walikuwa wakichukua vijiwe au changarawe zilizo moto (kwa jua) wakati wa sala ya adhuhuri na kuvipoza kwa kuvifikicha mikononi mwao. Vile vile utaziona hadithi zionyeshazo kwamba haijuzu kwa mwenye kusali kutumia kitu kingine iwapo anaweza kusujudu juu ya vitu hivyo (vijiwe au changarawe) baada ya kuondoa ule udhuru (wa joto au baridi) kwa kuvipooza (au kuvipasha moto).

Pia utakuta hadithi zionyeshazo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa akitandika nguo chini ya mikono yake inapotukia kuwa vijiwe na changarawe vimoto (sana) au vibaridi (mno). Hadithi hii imekomea hapa bila kueleza kwamba alikuwa akitandika mahali pa kusujudia au alikuwa akisujudu juu ya nguo. Kwa hivyo, inathibitika kwamba hairuhusiwi kusujudu juu ya kitu kisichokuwa ardhi.

Na inapokuwa hayumkiniki kusujudu juu ya ardhi kwa sababu ya joto jingi la kuumiza au udhuru wowote, hapo hakuna kizuizi kusujuau juu ya kitu kingine, kwani udhuru haufuati kanuni.

Pia hadithi nyingi zimepokewa kuhusu kusali juu ya mkeka, msala, busati n.k. ambazo humruhusu mwenye kusali kusujudu juu ya kila kiotacho katika ardhi, ilimradi tu kisiwe chenye kuliwa au kuvaliwa.

Hakika hakuna kitu kilicho bora kwa kusujudia mbele ya Mola wetu chenye kuleta unyenyekevu na udhalilifu mbele ya ukuu na Utukufu wa Mwenyezi Mungu kama ardhi hii ambamo ndimo tulimotoka, tunamoishi na tunamopatia riziki yetu na ambamo humo humo tutarejea. Kwa kuwa mtu anaposujudu juu ya ardhi kipaji chake huingia vumbi na udongo, hujiona kuwa si kitu na humjia unyenyekevu na hujiona dhahili mbele ya Mola wake. Fahari ya ukabila, utaiiri na takabari, yote hayo yatamtoka na atajiona kuwa yu kiumbe dhaifu mbele ya Ukuu na Utukufu wa Mwenyezi Mungu. Sifa na fikara hizo hazitamjia kamwe mtu

mwenye kusali juu ya mazulia au misala ya hariri iliyosukwa na kupambwa kwa nakshi na rangi tofauti tofauti bali badala yake, huweza kumletea takabari, majivuno na kujiona.

Sasa tunakuleteeni wasomaji wetu watukufu hadithi zilizonukuliwa katika vitabu sita maarufu viitwavyo "*As-Sihahu as-Sitta*" (ambavyo ni *Sahih Bukhari, Sahih Muslim, Jami Tirmidhi, Sunan Nasai, Sunan Ibn Majah* na *Sunan Abi Daud*) vyenye kutegemewa sana na pia vitabu vingine vinavyokubaliwa na ndugu zetu wa Kisunni. Vyote hivyo vinaonyesha sunna za Mtukufu Mtume (s.a.w.w) juu ya vitu vinavyojuzu kusujudia. Tunamwomba Mola atupe mwangaza wake wa kutuwezesha kufuata sunna zake zisizobadilika kabisa na kuzifanya kuwa mwongozo wetu. Hadithi zenyewe zimegawiwa sehemu tatu.

SEHEMU YA KWANZA : HADITHI ZITHIBITISHAZO KUWA NI WAJIBU KUSUJUDU KATIKA ARDHI

Hadithi zithibitishazo kuwa ni wajibu kusujudu katika ardhi:

Kwanza, hebu tuanze na zile Hadithi zinazothibitisha kuwa ni lazima kusujudu katika ardhi.

(1) Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amesema: "Mwenyezi Mungu amenifanyia ardhi kuwa mahali pa kusujudia na tohara."

جُعِلَتْ لِيَ الْأَرْضُ مَسْجِداً وَطَهُوْراً

Imam Muslim amepokea Hadithi isemayo hivi:
"Tumefanyiwa ardhi nzima kuwa mahali pa kusujudia na udongo wake tumefanyiwa tohara ikiwa tutakosa maji."

جعلت لنا الأرض كلها مسجدا، وجعلت تربتها لنا طهورا إذا لم نجد الماء

Imam Tirmidhi amepokea Hadithi isemayo hivi:
“Nimefanyiwa ardhi yote kuwa mahali pa kusujudia na tohara.”

جعلت لي الأرض كلها مسجدا وطهورا

Hadithi hii imepokewa pia na Mabwana Ali, Abdullah bin Umar, Abu Hurayrah, Jabir, Ibne Abbas, Hudhaifa, Anas, Abi Amama na Abu Dhar.

Bwana Bayhaqi amepokea Hadithi isemayo hivi:
“Nimefanyiwa ardhi tohara na mahali pa kusujudia.”

جعلت لي الأرض طهورا ومسجدا

Vile vile Bwana Bayhaqi amepokea Hadithi kwa namna nyingine isemayo kuwa: “Nimefanyiwa ardhi (kuwa ni) safi na mahali pa kusujudia. Na popote unapomfikia mtu wakati wa kusali, basi asali (mahali hapo) alipo.”[5]

جعلت لي الأرض طيبة ومسجدا، وأيما أدركته الصلاة صلى حيث كان

(2) Mtume Mtukufu (s.a.w.w) alimwambia sahaba mmoja Bwana Abu Dhar: “Ardhi ni mahali pa kusujudia wewe, basi popote unapokufikia wakati wa kusali sali.”[6]

الأرض لك مسجد فحيثما أدركت الصلاة فصل

(3) Shahaba mmoja Bwana Ibnu Abbas amesema: “Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisujudu juu ya kijiwe.”[7]

---

5 *Sahih Bukhari* cha Imam Muhammad bin Ismail Bukhari, Juzuu ya Kwanza, Uk. 86 na 113; *Sahih Muslim* cha Imam Muslim bin Hajjaj Naysaburi, Juzuu ya Pili, Uk. 64; *Sahih (Sunan) Nasai* cha Imam Abu Abdir Rahman Ahmad bin Shuaib Nasai, Juzuu ya Pili, Uk. 32; *Sahih (Sunan) Abu Daud* cha Imam Abu Daud Sulaiman bin as-Sajistani, Juzuu ya Kwanza, Uk. 79; *Sahih Tirmidhi* cha Imam Abu Isa Muhammad bin Isa as-Sulami at-Tirmidhi, Juzuu ya Pili, Uk. 114; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 433 na 435.

6 *Sahih (Sunan) Nasai*, Juzuu ya Pili, Uk. 32;

7 *Al-Mustadrak alaa al-Sahihain* cha Sheikh Muhammad bin Abdallah al-Hakim al-Nishapuri, Juzuu ya Tatu, Uk. 473.

ابن عباس: إن النبي (صلى الله عليه وآله وسلم) سجد على الحجر

Hadithi hii imepokewa na Bwana Hakim na kusadikishwa na Bwana Dhahabi.

(4) Sahaba mmoja Bwana Abu Said al-Khudri amesema: "Kwa macho yangu nilimwona Mtukufu Mtume (s.a.w.w), na kwenye pua na katika paji lake (la uso) palikuwepo alama za maji na udongo."[8]

أبصرت عيناي رسول الله (صلى الله عليه وسلم) وعلى أنفه وجبهته أثر الماء والطين

Hapana shaka kwamba alama hizi zilionekana wakati alipokuwa amekwisha sujudu juu ya ardhi.

(5) Sahaba mmoja Bwana Rufaa bin Raafi amesema: "Kisha (mwenye kusali) hutakbira na kusujudu, tena huweka paji lake juu ya ardhi mpaka kiwiliwili chake kinyooke na kitulie."[9]

ثم يكبر فيسجد فيمكن جبهته من الأرض حتى تطمئن مفاصله وتستوي

Hadithi hii imepokewa na Bwana Bayhaqi.

(6) Mabwana Al-Bazzaaz na Tabarani wamepokea hadithi yenye sanadi sahihi iliyosimuliwa na Mabwana Ibne Abbas, Anas na Baraydah isemayo kwamba moja katika mambo matatu yasiyofaa (katika Sheria) ni: "Mtu kupangusa udongo katika paji lake la uso kabla ya kumaliza sala yake."

ابن عباس، وأنس، وبريدة بإسناد صحيح مرفوعا: ثلاثة من الجفاء: يمسح جبهته قبل أن يفرغ من صلاته

8 *Sahih Bukhari*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 163 na 198; Juzuu ya Pili, Uk. 253, 254, 256, 258 na 259; *Sunan Abu Daud*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 143-144; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 104.

9 *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 102.

Na kufuatana na maneno ya Sahaba mmoja Bwana Waathila bin al-Asqaa kama yalivyopokewa na Mabwana Tabarani na Al-Bazzaaz, mojawapo ya hayo ni kwamba: “Mtu asipanguse paji lake (la uso kuonaoa) udongo mpaka amalize kusali.”[10]

وفي لفظ واثلة بن الأسقع: لا يمسح الرجل جبهته من التراب حتى يفرغ من الصلاة

(7) Sahaba mmoja Bwana Jabir bin Abdalla Ansari amesema: “Nilikuwa nikisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) sala ya adhuhuri, basi nikachukua fungu la vijiwe mkononi mwangu ili vipowe na niweze kusujudu juu yake kwa jinsi joto lilivyokuwa kali.”[11]

كنت أصلي مع رسول الله (صلى الله عليه وسلم) الظهر فآخذ قبضة من حصى في كفي لتبرد حتى أسجد عليه من شدة الحر

Imam Ahmad bin Hambal amepokea hadithi hiyo kwa maneno tofauti kidogo: “Tulikuwa tukisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.) sala ya adhuhuri, basi nikachukua fungu la vijiwe katika mkono mmoja na kuviweka katika mkono wa pili ili vipoe kutokana na joto jingi, kisha nikavisujudia.”[11]

كنا نصلي مع رسول الله (صلى الله عليه وسلم) صلاة الظهر، وآخذ بيدي قبضة من حصى فأجعلها في يدي الأخرى حتى تبرد ثم أسجد عليها من شدة الحر

Bwana Bayhaqi amepokea hivi: “Nilikuwa nikisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) sala ya adhuhuri, basi nikachukua fungu la vijiwe mkononi mwangu ili vipoe kutokana na joto jingi, kisha nikaviweka mahali pa kusujudia na nikasujudia.”[11]

---

10 *Majma’ul-Zawaid* cha Bwana Ibni Hajar-Al-Makki Uk. 83-84

11 *Musnad* cha Imam Ahmad bin Hambal, Juzuu ya Kwanza, Uk. 327; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 105.

كنت أصلي مع رسول الله (صلى الله عليه وسلم) صلاة الظهر فآخذ قبضة من الحصى في كفي حتى تبرد، وأضعها بجبهتي إذا سجدت من شدة الحر

Bwana Bayhaqi anaeleza kwamba Sheikh amesema, “Lau ingelijuzu kwa mwenye kusali kusujudu juu ya nguo aliyovaa basi ingekuwa rahisi zaidi kuliko kuvipoza vijiwe mikononi na baadaye kusujudu juu yao. Na tunamwomba Mwenyezi Mungu (atupe) Taufiki.”[11]

قال الشيخ: ولو جاز السجود على ثوب متصل به لكان ذلك أسهل من تبريد الحصى في الكف ووضعها للسجودعليها، وبالله التوفيق

(8) Sahaba mmoja Bwana Anas bin Malik amesema: “Tulikuwa tukisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) katika siku za joto kali, basi kila mmoja wetu (masahaba) akichukua vijiwe mkononi mwake ili kuvipoza na baadaye akaviweka kusujudia.”[12]

كنا نصلي مع رسول الله (صلى الله عليه وسلم) في شدة الحر فيأخذ أحدنا الحصباء في يده فإذا برد وضعه وسجدعليه

(9) Sahaba mmoja Bwana Khabab bin Al-Art amesema: “Tulimlalamikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kuhusu joto la ardhi linavyounguza vipaji (vya nyuso) na viganji vyetu, lakini (Mtukufu s.a.w.w) hakutujali.”[13]

شكونا إلى رسول الله (صلى الله عليه وسلم) شدة الرمضاء في جباهنا وأكفنا فلم يشكنا

12 *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 106

13 *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 105, 107; *Naylul Awtaar* cha Bwana Shawkani, Juzuu ya Pili, Uk. 268

(10) Sahaba mmoja Bwana Umar bin Khattab amesema: “Usiku mmoja ilinyesha mvua kisha tukatoka kwenda kusali sala ya asubuhi, basi kila mmoja wetu akachukua vijiwe mfukoni mwake na kuvitandika ili asali juu yao. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alipotuona tukifanya hivyo, alisema, ‘Uzuri ulioje wa busati hilo!’ Basi huo ulikuwa mwanzo wa kutumia vijiwe.”[14]

مطرنا من الليل فخرجنا لصلاة الغداة فجعل الرجل يمر على البطحاء فيجعل في ثوبه من الحصباء فيصلي عليه، فلما رأى رسول الله (صلى الله عليه وسلم) ذاك قال: ما أحسن هذا البساط. فكان ذلك أول بدء الحصباء

Bwana Abu Daud amenakili maneno ya Bwana Ibne Umar akisema: “Usiku mmoja ilinyesha mvua na ardhi ikawa chepechepe. Basi kila mmoja akachukua vijiwe kutoka katika nguo yake na kuvitandika chini yake.”[14]

مطرنا ذات ليلة فأصبحت الأرض مبتلة فجعل الرجل يأتي بالحصى في ثوبه فيبسطه تحته، الحديث

(11) Sahaba mmoja Bwana Ayadh bin Abdallah Al-Qarashi amesema: “Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w.) alimwona mtu mmoja akisujudu juu ya kunjo la kilemba kilichoshuka kwenye paji lake (la uso). Mtume akamwashiria kwa mkono wake, ‘Ondoa kilemba chako.’”[15]

رأى رسول الله (صلى الله عليه وسلم) رجلا يسجد على كور عمامته فأومأ بيده: ارفع عمامتك، وأومأ إلى جبهته

(12) Imam Ali Amirul-Mu’miniyn amesema: “Ikiwa mmoja wenu anasali basi aondoe kilemba chake kwenye paji lake (la uso).”[15]

14 *Sunan Abu Daud*, Juzuu ya Kwana, Uk. 75; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 440

15 *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 105

إذا كان أحدكم يصلي فليحسر العمامة عن جبهته

(13) Sahaba mmoja Bwana Naafi' amesema kwamba wakati Abdallah bin Umar anaposujudu akiwa na kilemba basi hukitenga na paji lake la uso ili (paji lake) likae juu ya ardhi."[15]

إن عبد الله بن عمر كان إذا سجد وعليه العمامة يرفعها حتى يضع جبهته بالأرض

(14) Sahaba mmoja Bwana Abada bin As-Saamit anaposimama kusali huondoa kilemba kwenye paji lake la uso.[15]

عبادة بن الصامت إنه كان إذا قام إلى الصلاة حسر العمامةعن جبهته

(15) Sahaba mmoja Bwana Abu Ubaida amesema: "Ibne Masuud alikuwa hasali wala kusujudu isipokuwa juu ya ardhi tu."[16]

إن ابن مسعود كان لا يصلي أو لا يسجد إلا على الأرض

Hadithi hii imenukuliwa na Bwana Tabarani katika kitabu chake kiitwacho *Al-Maj-ma'ul Kabir*.

(16) "Ibrahim alikuwa akisimama kusali juu ya 'al-Burdii' na akisujudu juu ya ardhi. Tukamwuliza, 'Al-Burdii' ni kitu gani? Akajibu, ni 'Mafunjo' (aina ya majani)."[16]

إبراهيم إنه كان يقوم على البردي ويسجد على الأرض. قلنا: ما البردي؟ قال: الحصير

(17) Sahaba mmoja Bwana Saleh bin Haywan as-Sabaai amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimwona mtu mmoja akisujudu ubavuni mwake na kilemba chake kilikuwa kimefunika paji lake la uso, basi Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akakiondoa kwenye paji lake."[17]

16 *Al-Majma* cha Bwana Ibnil Hajar Haythami Shaykhani, Juzuu ya Pili, Uk. 57

17 *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 105; *Nasbur-Raayah* cha Bwana Zaylai, Juzuu ya Kwanza, Uk. 386

إن رسول الله (صلى الله عليه وسلم) رأى رجلا يسجد بجنبه وقد اعتم على جبهته فحسر رسول الله (صلى الله عليه وسلم) عن جبهته

SEHEMU YA PILI : HADITHI ZINAZORUHUSU KUSUJUDU KATIKA VITU VINGINEVYO

Sasa hebu tuzijie Hadithi zinazoruhusu kusujudu katika vitu vinginevyo badala ya ardhi pasi na udhuru wowote:-

(1) Sahaba mmoja Bwana Anas bin Malik amesema: "Bibi yangu Malika alimwalika Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kula chakula nyumbani kwake, basi akala chakula. Ulipofika wakati wa sala, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akasema, 'Amkeni nikusalisheni'."

Anas akaendelea kusema:- "Nikauleta mkeka mkuukuu na kuwa mweusi kwa kutumika sana; kisha nikaulowesha kwa kuunyunyizia maji, tena hapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akasimama, nami nikajipanga katika safu, yatima mmoja nyuma yake na kizee mmoja nyuma yetu."[18]

إن جدته مليكة دعت رسول الله (صلى الله عليه وسلم) لطعام صنعته له فأكل منه ثم قال: قوموا فلأصلي لكم، قال أنس: فقمت إلى حصير لنا قد اسود من طول ما لبس، فنضحته بماء، فقام رسول الله (صلى الله عليه وسلم)، وصففت، واليتيم وراءه، والعجوز من ورائنا. الحديث

Bwana Anas amesema: "Umme Saliym alimwomba Mtukufu Mtume (s.a.w.) afike kwake na kusali nyumbani mwake ili mahali hapo pawe ni msala wake. Basi (Mtume s.a.w.) akafika, na yule bibi akaleta mkeka akaunyunyizia maji, kisha (Mtume) akasimama

18 *Sahih Bukhari*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 101.

kusali na wenyeji wakasali pamoja naye."[19]

إن أم سليم سألت رسول الله (صلى الله عليه وسلم) أن يأتيها فيصلي في بيتها فتتخذه مصلى فأتاها فعمدت إلى حصير فنضحته بماء فصلى عليه وصلوا معه

Bwana Anas amesema: "Mmoja katika ami zangu alitayarisha chakula na kumwomba Mtukufu Mtume (s.a.w.w), kwa kusema, 'Napenda ule nyumbani mwangu na usali humo.' Basi (Mtume s.a.w.w) akaja na nyumbani humo mlikuwemo 'fahal'. (Mtume s.a.w.w) akaamrisha upande mmoja wa hiyo (fahal) ufagiliwe na unyunyuziwe maji; kisha akasimama kusali nasi tukasali naye."
Bwana Ibne Majah amesema: 'Fahal' ni mkeka mkuukuu na ambao umekuwa mweusi kwa kutumika sana."[20]

صنع بعض عمومتي للنبي طعاما فقال للنبي (صلى الله عليه وسلم): إني أحب أن تأكل في بيتي وتصلي فيه قال: فأتاه وفي البيت فحل من هذه الفحول فأمر بناحية منه فكنس ورش فصلى وصلينا معه.
فقال: قال أبو عبد الله بن ماجة: الفحل هو الحصير الذي قداسود

Bwana Anas amesema: "Alipokuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) akilala wakati wa 'Qaylula' (nusu ya mchana) kwa Umme Saliym alikuwa akimtandikia kirago cha ngozi na akiyakusanya majasho yaliyokuwa yakimtoka (Mtume s.a.w.w) na kuyatia katika mrashi wake na akimtandikia jamvi alilokuwa akisalia."[21]

كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) يقيل عند أم سليم فتبسط له نطعا فتأخذ من عرقه فتجعله في طيبها، وتبسط له الخمرة ويصلي عليها

Bwana Anas amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa mwenye tabia njema kuliko watu wote. Ikiwa wakati wa sala umefika naye

19 *Sahih Nasai*, Juzuu ya Pili, Uk. 57
20 *Sunan Ibne Majah*, cha Imam Ibn Majah al-Qazwini, Juzuu ya Kwanza, Uk. 255
21 *Sunanul Bayhaq*i cha Imam Ahmad bin Husain bin Ali al-Bayhaqi, Juzuu ya Pili, Uk. 421

yupo nyumbani, basi huamrisha mkeka uliopo chini yake ufagiliwe na unyunyiziwe maji. Kisha husimama nasi tukasimama nyuma yake kutusalisha. Mikeka yao husukwa kwa majani mabichi ya mtende."[22]

Bwana Anas amesema pia: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) aliingia katika nyumba moja yenye busati la mtende, kisha akalifagia upande mmoja, akarashia maji na akasali juu yake".

Katika pembezoni mwa ukurasa wa kitabu kiitwacho '*Sananul Kubra*' (inaojulikana kama *Sunanul Bayhaqi*) imeelezwa hivi: "Al-Fahal" ni busati (mkeka) uliosukwa kutokana na makuti mabichi ya mitende dume".
كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) أحسن الناس خلقا فربما تحضره الصلاة وهو في بيتنا فيأمر بالبساط الذي تحته فيكنس ثم ينضح ثم يقوم فنقوم خلفه فيصلي بنا. قال: وكان بساطهم من جريدالنخل.
وفيه أيضا لفظ: إن رسول الله (صلى الله عليه وسلم) دخل بيتا فيه فحل فكسح ناحية منه ورش فصلى عليه.
قال في هامش السنن: الفحل: حصير معمول من سعف فحال النخل.

Vili vile Imam Tirmidhi amepokea hadithi hii kutoka kwa Anas akisema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w) akalinyunyuzia maji busati letu na akasali juu yake."[23]
ملخصا: عن أنس قال: نضح بساط لنا فصلى عليه.

(2) Sahaba mmoja Bwana Abbas amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa akisali juu ya 'Khumra.'"[24]

Imam Tirmidhi anasema kwamba Imam Ibnul Arabi al-Maliki (ambaye ni mmoja katika viongozi mashuhuri wa Kisunni)

22 *Sunanul Bayhaq*i, Juzuu ya Pili, Uk. 436
23 *Sahih Tirmidhi*, Juzuu ya Pili, Uk. 128.
24 *Sahih Tirmidhi*, Juzuu ya Pili, Uk. 126.

amesema: "'Khumra' ni mkeka mdogo wa kusalia."

كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) يصلي على الخمرة

قال الإمام ابن العربي المالكي: الخمرة: حصير الصلاة.

(3) Sahaba mmoja Bwana Abu Said Al-Khudri amesema: "Nilikwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) nikamkuta anasali juu ya mkeka na akisujudu juu yake."[25]

أبو سعيد الخدري: أنه دخل على النبي (صلى الله عليه وسلم)، فرأيته يصلي على حصير يسجد عليه

Katika kitabu kiitwacho '*Jamiah*' Juzuu ya Pili Uk. 127 cha Bwana Tirmidhi, hakuna maneno haya: "Na akisujudu juu yake."

(4) Bibi Maymuna Ummul-Mu'miniyn (mke Mtukufu wa Mtume s.a.w.) amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alipokuwa akisali, nami nilikuwa nikisali ubavuni mwake; pengine nguo yake hunigusa anaposujudu; naye alikuwa akisali juu ya khumra."[26]

ميمونة أم المؤمنين: كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) يصلي وأنا حذائه وربما أصابني ثوبه إذا سجد، وكان يصلي على خمرة

Bibi Ayesha amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) ameniambia, 'Niletee khumra kutoka msikitini'. Nikamjibu, 'Mimi nina hedhi'. Akanijibu, 'Hedhi haimo katika mikono yako."[27]

عن عائشة قالت: قال لي رسول الله (صلى الله عليه وسلم): ناوليني الخمرة من

25 *Sahih Muslim*, Juzuu ya Pili, Uk. 62 na 128; *Sunan Ibne Majah*, Juzuu ya Pili, Uk. 321.

26 *Sahih Bukhari*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 101; *Sahih Muslim*, Juzuu ya Pili, Uk. 128; *Sunan Ibne Majah*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 320; *Sahih Nisai*, Juzuu ya Pili, Uk. 57; *Sunanul Bayhaqi*, Juzuu ya Pili, Uk. 421;

27 *Sahih Muslim*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 168

المسجد قالت: فقلت: إني حائض فقال: إن حيضتك ليست في يدك.

(5) Sahaba mmoja Bwana Ibne Umar amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikliwa akisali juu ya khumra na akisujudu juu yake."[28]

ابن عمر: كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) يصلي على الخمرة ويسجد عليها

(6) Bibi Umme Salmah Ummul-Mu'miniyn amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa na busati na khumra na (alikuwa) akisalia juu yake."[29]

أم سلمة أم المؤمنين: كان لرسول الله حصير وخمرة يصلي عليها

Hadithi hii imeelezwa na Bwana Abu Ya'la na Bwana Tabarani ameinakili katika vitabu viitwavyo *Al-Kabir* na *Al-Awsat*. Wapokezi waliotajwa na Abu Ya'la ni waaminifu. Hadithi kama hii imenakiliwa pia kutoka kwa Bibi Umme Habiba.

(7) Sahaba mmoja Bwana Anas amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa akisali juu ya khumra na akisujudu juu yake."[30]

أنس: كان رسول الله (صلى الله عليه وسلم) يصلي على الخمرة ويسجد عليها

SEHEMU YA TATU
HADITHI ZINAZORUHUSU KUSUJUDU KATIKA VITU VINGINEVYO KWA UDHURU FULANI

Sasa hebu na tumalizie kwa kuzitazama zile Hadithi zinazomruhusu mtu kusujudu katika vitu vinginevyo visivyo ardhi iwapo mtu atakuwa na udhuru fulani:-

28 *Al-Kabir* cha Imam Abul-Qasim Sulaiman bin Ahmad Tabarani, na *Al-Awsat* cha Imam Abul-Qasim Sulaiman bin Ahmad Tabarani.

29 *Al-Majma*, Juzuu ya Pili, Uk. 57.

30 *Al-Awsat* na *As-Saghiyr* cha Imam Abul-Qasim Sulaiman bin Ahmad Tabarani.

(1) Sahaba mmoja Bwana Anas bin Malik amesema: “Tulipokuwa tukisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w), kila mmoja wetu alikuwa hajimudu kuweka paji la uso juu ya ardhi kwa sababu ya joto kali, hivyo kila mmoja aliweka vazi lake na akasujudia.”[31]

أنس بن مالك: كنا إذا صلينا مع النبي صلى الله عليه وسلم فلم يستطع أحدنا أن يمكن جبهته من الأرض من شدة الحر طرح ثوبه ثم سجدعليه

Imam Bukhari amepokea hivi: “Tulipokuwa tukisali na Mtukufu Mtume (s.a.w.), baadhi yetu tuliweka sehemu ya mavazi yetu mahali pa kusujudia kwa sababu ya joto kali.”[31]

وفي لفظ البخاري: كنا نصلي مع النبي صلى الله عليه وسلم فيضع أحدنا طرف الثوب من شدة الحر في مكان السجود

Imam Muslim amepokea hivi: “Tulipokuwa tukisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.) kila mmoja wetu asiyeweza kuweka paji lake la uso juu ya ardhi kwa sababu ya joto kali, aliweka sehemu ya vazi lake (mahali pa kusujudia) na akasujudia.”[31]

وفي لفظ مسلم: كنا نصلي مع النبي صلى الله عليه وسلم في شدة الحر فإذا لم يستطع أحدنا أن يمكن جبهته من الأرض بسط ثوبه فسجد عليه

Pia Hadithi hii imesimuliwa kwa namna hii: “Tulipokuwa tukisali pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.) baadhi yetu waliweka sehemu ya mavazi yao mahali pa kusujudia kwa sababu ya joto kali.”[31]

وفي لفظ: كنا إذا صلينا مع النبي صلى الله عليه وسلم فيضع أحدنا طرف الثوب من شدة الحر مكان السجود

31 *Sahih Bukhari*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 101; *Sahih Muslim*, Juzuu ya Pili, Uk. 109; *Sunan Ibne Majah*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 321; *Sunan Abu Daud*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 106; *Sunanul Darimiy,* Juzuu ya Kwanza, Uk. 308; *Musnad* Ahmad Ibne Hambal, Juzuu ya Kwanza, Uk. 100; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 106; *Naylul Awtaar*, Juzuu ya Pili, Uk. 268.

Bwana Shawkani katika kitabu chake kiitwacho *Naylul Awtaar* amesema: “Hadithi hiyo iliyotajwa hapo juu inaonyesha kwamba kusujudu juu ya vazi (nguo) kwa sababu ya kujikinga kutokana na joto la ardhi huruhusiwa. Hii inaonyesha kwamba madhumuni hasa ni kusujudu juu ya ardhi, kwa sababu kusujudu juu ya vazi kunaruhusiwa pale tu mtu anapokuwa hawezi kustahimili joto la ardhi. Ili kumruhusu mwenye kusali kusujudu katika vazi lake, wanavyuoni wametumia hadithi hii kuwa hoja (yao).”

Bwana Nawawi anasema kwamba *Fatwa* ya Abu Hanifa na wanavyuoni wengi ni kama hiyo.

قال الشوكاني في النيل: الحديث يدل على جواز السجود على الثياب لاتقاء حر الأرض، وفيه إشارة إلى أن مباشرة الأرض عند السجود هي الأصل، لتعليق بسط ثوب بعدم الاستطاعة، وقد استدل بالحديث على جواز السجود على الثوب المتصل بالمصلي

قال النووي: وبه قال أبو حنيفة والجمهور.

(2) Sahaba mmoja Bwana Anas bin Malik amesema: “Tulipokuwa tukisali adhuhuri (‘adh-dhahaair’) nyuma ya Mtukufu Mtume (s.a.w.), tulisujudujuu ya mavazi yetu ili kujilinda na joto.”[32]

أنس بن مالك: كنا إذا صلينا خلف رسول الله صلى الله عليه وسلم بالظهائر سجدنا على ثيابنا اتقاء الحر

Imam Sindi katika maelezo yake juu ya hadithi hii anasema, “Adh-dhahaair” ni wingi wa ‘dhihiyra’ (adhuhuri) na maana yake ni wakati wa joto kali (katika) nusu ya mchana. Ni dhahiri kwamba maneno “tulisujudu juu ya mavazi yetu” maana yake ni kwamba, mavazi waliyoyavaa ndiyo waliyoyasujudia, kwani wakuti huo nguo hazikuwa nyingi, hivyo walipata wapi nguo zaidi? Hii inathibitisha

32 *Sunan Ibne Majah*, Juzuu ya Pili, Uk. 216

kwamba inaruhusiwa kwa mwenye lrusali kusujudu juu ya vazi lake alilovaa tu, kama inavyokubaliwa na (wanavyuoni) wengi."

وقال الإمام السندي في شرحه: الظهائر جمع ظهيرة وهي شدة الحر نصف النهار (سجدنا على ثيابنا) الظاهر أنها الثياب التي هم لابسوها ضرورة أن الثياب في ذلك الوقت قليلة، فمن أين لهم ثياب فاضلة؟ فهذا يدل على جواز أن يسجد المصلي على ثوب هو لابسه كما عليه الجمهور.

Maelezo hayo wanayatoa kufuatana na masimulizi ya Bwana Ibne Abbas akisema: "Nilimshuhudia Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisali na kusujudu juu ya vazi lake."

وعلى هذه الصورة يحمل ما جاء عن ابن عباس: رأيت رسول الله يصلي يسجد على ثوبه

Hadithi hii imepokewa na Bwana Abu Ya'la na Bwana Tabarani katika kitabu chake kiitwacho *Al-Kabir*.

Bwana Bukhari katika kitabu chake kiitwacho *Sahih* mlango wa "Kusujudia Vazi Wakati wa Joto Kali", ananakili (maneno ya Bwana) Hasan akisema: "Watu walikuwa wakisujudu juu ya vilemba na kofia zao na mikono yao wakiitia katika mikono ya mavazi yao."[33]

وقال الحسن: كان القوم يسجدون على العمامة والقلنسوة ويداه في كمه

Tanabahi:

Kuna hadithi moja iwafanyayo wanavyuoni kuchukulia kuwa inajuzu kusujudu juu ya vazi inapotokea udhuru ijapokuwa katika hadithi hiyo kusujudu katika vazi hakukutajwa hasa. Hadithi hiyo ni hii:

33 *Sahih Bukhari*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 101

Bwana Ibne Abbas amesema: “Asubuhi na mapema katika siku za baridi nilimwona Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisali juu ya kitambaa cheupe na huku akiiepusha mikono na miguu yake kutokana na baridi ya ardhi kwa Kitambaa hicho.”

عن ابن عباس: رأيت رسول الله صلى الله عليه وسلم يصلي في كساء أبيض في غداة باردة يتقي بالكساء برد الأرض بيده ورجله

Imam Ahmad bin Hambal amepokea hivi: “Siku moja ya mvua, nilimwona Mtukufu Mtume (s.a.w.) alipokuwa akisujudu, aliweka kitambaa alichojiviringishia chini ya mikono yake ili kujikinga na matope.”

وفي لفظ أحمد: لقد رأيت رسول الله صلى الله عليه وسلم في يوم مطير وهو يتقي الطين إذا سجد بكساء عليه يجعله دون يديه إلى الأرض إذا سجد

Bwana Thabit bin Saamit amepokea hivi: “Alipokuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisali katika msikiti wa Bani Abdul Ashhal, aliweka mikono yake juu ya kitambaa alichojiviringishia ili kujiepusha na baridi ya mawe.”

وعن ثابت بن صامت: إن رسول الله صلى الله عليه وسلم قام يصلي في مسجد بني عبد الأشهل وعليه كساء ملتف به يضع يده عليه يقيه برد الحصى

Hadithi hii pia imepokewa hivi: “Nilimwona (Mtume) wakati alipokuwa akisujudu, akiweka mikono yake katika vazi lake.”

وفي لفظ: رأيته واضعا يديه في ثوبه إذا سجد

Ibne Majah amepokea hivi: “Nilimwona (Mtume) wakati alipokuwa akisujudu, akiweka mikono yake juu ya vazi lake”.[34]

34 *Sunan Ibne Majah*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 321; *Sunanul Kubra*, Juzuu ya Pili, Uk. 108; *Nasbur Raayah*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 386; *Naylul Awtaar*, Juzuu ya Pili, Uk. 269-270.

وفي لفظ ابن ماجة: فرأيته واضعا يديه على ثوبه إذا سجد

Bwana Shawkani katika kitabu chake kiitwacho *Naylul Awtaar* anasema: "Hadithi hii inaonyesha kwamba inapokuwa kuna udhuru inaruhusiwa kwa mwenye kusali kujihifadhi pembezoni mwa nguo aliyoivaa. Udhuru huo ama ni mvua kama ilivyotajwa katika hadithi, au ni joto na baridi kama ilivyoelezwa katika hadithi na Ibne Abu Shaibah. Hadithi tunayoizungumzia inaonyesha dhahiri kwamba kitambaa alichokuwa akisujudia Mtukufu Mtume (s.a.w) kilikuwa ni kitambaa alichojitandia (alichovaa)."

قال الشوكاني في نيل الأوطار: الحديث يدل على جواز الاتقاء بطرف الثوب الذي على المصلي ولكن للعذر، إما عذر المطر كما في الحديث، أو الحر والبرد كما في رواية ابن أبي شيبة وهذا الحديث مصرح بأن الكساء الذي سجد عليه كان متصلا به.

Kwa maelezo haya, sisi hatuoni kuwa ni sahihi na sawa, kwa sababu hadithi yanaonyesha dhahiri kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akitumia nguo kwa kuhifadhi miguu na mikono yake tu wala hakuna ishara yoyote kwamba allkuwa akitumia kwa kusujudia au kwa kuwekea paji la uso. Mwishowe tunaweza kukubaliana juu ya hadithi ile ya Bibi Ayesha, nayo ni hii:

Bibi Ayesha amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) anaposali haweki kitu chochote chini ya miguu yake, isipokuwa siku moja iliponyesha mvua aliweka ngozi chini ya miguu yake."[35]

ونحن لم نر هذا الحمل في محله إذ الحديث لا يدل بظاهره إلا على اتقاء رسول الله (صلى الله عليه وآله وسلم) بالكساء برد الأرض بيده ورجله فحسب، وليس فيه إيعاز قط إلى السجدة والجبهة، وسبيله سبيل حديث السيدة عايشة:

35 *Sunanul Bayhaqi*, Juzuu ya Pili, Uk. 436

كان رسول الله إذا صلى لا يضع تحت قدميه شيئا إلا أنا مطرنا يوما فوضع تحت قدميه نطعا

Hadithi hii imepokewa na Bwana Tabarani katika kitabu chake kiitwacho *Al-Awsaat* na Bwana Bayhaqi. Bwana Haythami katika kitabu chake kiitwacho *Al-Majma* (Juzuu ya Pili, uk. 57) anaeleza kuwa hadithi hii ni dhaifu kwa sababu moja, mmoja wa wapokezi ni Ibrahim bin Ishaq Adh-Dhabii.

Pia kuna hadithi nyingine iliyotajwa na Imam Ahmad bin Hambal katika kitabu chake kiitwacho *Al-Musnad* kama ilivyopokewa kutoka 'Sanadi' (mfululizo wa majina ya wapokeaji wa Hadithi) ifuatayo:- Muhammad bin Rabia - Yunus bin Al-Harith At-Taifi - Abi Aun - (ambaye alipokea) kutoka kwa baba yake kwamba Sahaba (mmoja Bwana) Mughira bin Shuuba amesema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa akigenda kusali juu ya ngozi yenye manyoya iliyotiwa dawa ili isioze."[36]
عن محمد بن ربيعة عن يونس بن الحرث الطائفي عن أبي عون عن أبيه عن المغيرة بن شعبة قال: كان رسول الله صلى الله عليه وسلم يصلي أو يستحب أن يصلي على فروة مدبوغة

'Sanadi' ya hadithi hii ni dhaifu kabisa na haiwezekani kukubaliwa katika mambo ya kisheria, kwa sababu mmoja katika wapokezi wake ni Yunus bina Al-Harith at-Taifi, ambaye Ahmad bin Hambal ametaja kuwa: "Hadithi zake ni za ubishi.'

Bwana Abdalla bin Ahmad amesema: "Nilimwuliza (baba yangu) mara nyingine kuhusu mtu huyo akamtaja kwa sifa mbaya zaidi".

Bwana Ibne Mu'in amesema: "Hana maana".

36 *Musnad* cha Imam Ahmad bin Hambal, Juzuu ya Nne, Uk. 254; *Sunan Abu Daud*, Juzuu ya Kwanza, Uk. 106; *Sunanul Bayhaqi*, Juzuu ya Pili, Uk. 420.

Bwana Abu Hatim amesema: “Hategemewi”.

Imam Nasai amesema: “Hategemewi”. Na kwa mara ya pili, akasema: “Hana itibari”.

Bwana Ibn Abi Shaiba amesema: “Nilimwuliza Ibn Mu’in habari yake, akajibu, ‘Tulikuwa tukimwona kuwa si mtu wa kuamimka hata kidogo”.

Bwana As-Saaji amesema katika kitabu chake kiitwacho *Tahdhibut-Tahdhib*, Juzuu ya Kumi na Moja, Uk. 437 kuwa “Ndiyo, yeye si mtu wa kuaminiwa lakini hakusingiziwa kusema uwongo.”

Na pia katika sanadi ya hadithi hiyo yumo mtu aitwaye Abi Aun Ubaidullah bin Said Ath-Thaqafi Al-Kufi. Kama ilivyoelezwa katika kitabu cha *Al-Jurh-wat-Tadiyl*, Bwana Abu Hatim alimwambia mwanawe kwamba “Huyu (Abi Aun) hajulikani (ni nani).”

Bwana Ibne Hajar amesema: “Hadithi yake aliyoipokea kutoka kwa Mughira ni ‘*Mursal*’ (Maana yake ni kuwa, majina ya baadhi ya wapokeaji wake hayakutajwa).

Tukiachilia mbali hayo yote, na tukiangalia maneno ya Hadithi yenyewe tutaona kwamba kusujudu na hukumu zake havikutajwa bali kumetajwa tu kusali juu ya ngozi yenye manyoya wala hakuna neno lionyeshalo kusujudu juu yake.

UAMUZI WA HAKI

Hadithi hizi zote zimenakiliwa kutoka katika vitabu sita sahihi (*As-Sihahu as-Sitta*) na vitabu vya sanadi (*Masaanid*), ambavyo ni vitabu vya hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.) vyenye kutegemewa na vilivyotungwa na wanavyuoni wa Kisunni. Hadithi zote

zinazohusu mambo ya kusujudu kutoka vitabu hivyo tumezinakili wala hakuna hadithi ihusuyo jambo hilo tuliyoiacha.

Hadithi hizi zote zinazungumzia kuhusu kusujudu, na zinabainisha kwamba iwapo kuna uwezo na inayumkinika, basi mwenye kusali lazima asujudu juu ya ardhi, au juu ya vitu vinavyoota ardhini, au juu ya vitu vilivyotengenezwa kutokana na vitu viotavyo ardhini ambavyo vinaingia katika hukumu moja pamoja na ardhi, kama ilivyotajwa katika hadithi ihusuyo khumra, mkeka, busati, jamvi na kadhalika.

Wakati unapokuwa huna udhuru wowote itakubidi usujudu juu ya mojawapo katika vitu hivyo wala haijuzu kusujudu juu ya vitu vingine visivyokuwa hivyo.

Lakini mwenye kusali anapokuwa na udhuru wa kutoweza kusujudu juu ya ardhi, basi anaruhusiwa kusujudu juu ya nguo aliyoivaa tu wala si zile asizozivaa wakati ule; kwa sababu ruhusa ya kusujudu juu ya mavazi yasiyokuwa mwilini wakati wa kusali haikutajwa katika hadithi hiyo.

Ama kuhusu kusujudu juu ya matandiko, mazulia yaliyofumwa kwa hariri au kwa manyoya ya wanyama wa aina yoyote ile au juu ya kitambaa au vazi lisilokuwa mwilini, hakuna dalili wala uthibitisho wowote unaomruhusu kuvisujudia vitu hivyo, wala haikupokewa hadithi sahihi yenye kutegemewa inayoruhusu kuvisujudia vitu hivyo. Katika hivi vitabu sita sahihi na maarufu ambavyo hudhamini hukumu na maamrisho ya dini na hasa sala ambayo ni nguzo muhimu sana, hamna hata hadithi moja wala neno moja wala ishara au dokezo lionyeshalo ruhusa ya kusujudu vitu hivyo!!!

Vivyo hivyo, vitabu vingine vya hadithi vyenye kutegemewa (kama vile vitabu vya sanadi na sunnah) vilivyotungwa katika karne tatu za kwanza, vyote hivyo havina ushahidi hata katika hadithi za daraja la '*marfuu*' au '*mawquuf*' au '*musnad*' au '*mursal*' wenye

kuruhusu kusujudu juu ya vitu hivyo.

Kwa hivyo, ruhusa ya kusujudu juu ya matandiko, mazulia na misala iliyofumwa kwa hariri, manyoya n.k:, na pia kuendelea kusujudia vitu hivi msikitini (kama ilivyo kawaida ya watu wengi siku hizi) ni jambo lililozushwa ambalo linapinga sunna za Mwenyezi Mungu na Mtume wake (s.a.w.), ambapo kwa hakika Mwenyezi Mungu anatuambia:-
"... Lakini hutapata mabadiliko katika kawaida (sunna) ya Mwenyezi Mungu wala hutakuta mageuko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu." (Qur'ani, 35:43).

Katika kitabu kiitwacho *Al-Musannif*, juzuu ya pili, mwanachuoni mashuhuri wa Kisunni Bwana Al-Hafidh Al-Kabir Abu Bakr bin Abu Shaiba amepokea masimulizi kutoka kwa Bwana Said bin Musayyib na Bwana Muhammad bin Siyriyn kwamba: "Kusali juu ya zulia ni jambo lililozushwa (*bid'a*), (baada ya Mtukufu Mtume s.a.w.)." Ama kuhusu *bid'a* katika sunna za Mtukufu Mtume (s.a.w.), imepokewa hadithi sahihi inayokubaliwa na Waislamu wote, kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema: "Mambo mabaya kabisa (katika dini) ni uzushi, na kila uzushi ni *bid'a* (mageuzi ya dini)."

KUSUJUDU KATIKA UDONGO WA KARBALA

Lengo hasa la Shia kuufanya udongo wa Karbala kuwa ni mahali na kitu cha kusujudia linashikana na misingi miwili madhubuti.

Msingi wa Kwanza:
Kupata udongo wa kusujudia ulio tohara popote pale mtu awapo.

Ni bora kwa mwenye kusali ajitahidi wakati anapotaka kusali mbele ya Mola wake kupata udongo wa kusujudia ambao ana uhakika nao kuhusu utohara na usafi wake. Haidhuru ikiwa udongo huo a

meuchukua kutoka katika ardhi yoyote ile au mahali popote pale, duniami. Kisheria, ardhi yote ni moja ikiwa tu udongo uliochukuliwa kwa ajili ya kusujudia ni tohara, wala hakuna tofauti kati ya udongo wa mahali mbali mbali.

Kwa kufuatana na sheria, mwili wa mwenye kusali, nguo zake na mahali anaposali lazima viwe tohara, hususan anapokuwa safarini, kwani ni vigumu kuhakikisha utohara wa ardhi ngeni ambayo ataweza kusujudia. Je, itayumkinika vipi kwa msafiri kuhakikisha utohara wa mahali anapokuwepo kama vile hotelini, barabarani, na katika vituo vya mabasi, stesheni za gari moshi na kadhalika, wakati anajua kwamba mahali hapo wapo kila aina ya watu, Waislamu na wasio Waislamu ambao hawajali maamrisho ya dini kuhusu utohara na unajisi?

Basi kuna pingamizi gani kwa Mwislamu mwenye imani achukuaye hadhari katika mambo yake ya kidini ikiwa daima atakuwa na udongo alio na hakika nao kuhusu utohara wake ili aweze kusujudia mahali popote aendako?

Je, kwa kufanya hivyo, hataepukana na kusujudu juu ya uchafu au mahali pasipo tohara patakapoifanya sala yake kutokubaliwa wala kupata ukaribu na Mola wake?

Na kwa kuzingatia maagizo yote ya sheria kuhusu utohara wa mwili na nguo za mwenye kusali, na kukatazwa kusali mahali kama vile jaani, machinjoni, makaburini, mazizini, barabarani na hamamuni, na baada ya kuyazingatia maamrisho ya kuweka misikiti katika hali unadhifu na utohara, je.,mwenye akili kamili yupi atasali mahali pasipo tohara na nadhifu? (Tazama kitabu kiitwacho *Sunan* cha Bwana Ibne Majah, Juzuu ya Kwanza, Uk. 252 na 256).

Fikara nzuri hii ya ukweli na unyofu wa kidini ilikuwa ikifuatwa na wachamungu na wanavyuoni wa zamani katika karne ya

kwanza ya Uislamu. Kwa mfano, yule mtu aliyekuwa akiishikilia na kuifuata sana sunna hii nzun alikuwa Bwana Masrouq bin Al-Adja at-Tabiey, mwanachuoni mashuhuri ambaye anakubaliwa na Waislamu wote. Kwa kuishikilia sunna hii nzuri, alikuwa akichukua kipande cha udongo ('labinah') kwa kusujudia katika safari zake. Bwana Abu Bakr bin Abu Shaiba mwanachuoni wa Kisunni mashuhuri sana katika zama zake, alisema katika kitabu chake kiitwacho *Al-Musannif*, Juzuu ya Pili, chini ya mada "Wenye Kuchukua Kitu cha Kususanadi mbili" kwamba: 'Kila (Bwana) Masrouq alipokuwa akisafiri kwa jahazi alikuwa akichukua kipande cha udongo na akikisujudia."

Huu ndio msingi wa kwanza wanaoutegemea Mashia. Vile vile ni msingi wa asili wa masahaba wa awali na Tabiin (masahaba wa masahaba wa Mtume s.a.w.).

Msingi wa Pili:
Kupata udongo uhusianao zaidi na Mwenyezi Mungu.

Hapana shaka kuwa, (kupata udongo uhusianao zaidi na Mwenyezi Mungu) kufuatana na akili na kanuni za kawaida lazima uwepo ubora kati ya ardhi (nchi) mbali mbali ambao unategemea namna uhusiano wake na Mwenyezi Mungu ulivyo."[37]

Kwa hivyo, ubora wa ardhi fulani unatokana na asili yake, maoni

37 Uhusiano baina ya chombo na mwenye chombo unapatikana kwa kuongeza kihusisho kiletacho maana na taswira au ubora utarajiwao. Kwa mfano, sentensi "Nyumba Mungu" haileti maana yoyote wala haikamilishi taswira. Lakini tunapoongeza kihusisho 'ya' baina ya chombo (yaani nyumba) na mwenye chombo (yaani Mungu), uhusiano baina yao unaopatikana na kujulikana ni "Nyumba ya Mungu." Na kwa kihusisho hicho ya (aa wa, cha, vya, la na za kama kinavyotumika katika lugha) uhusiano hupatikana. Hivyo, chombo kinapokuwa ni cha Mungu huwa na sifa na ubora mahsusi. Hivyo hivyo, vyombo vyote vingine vinapata uhusiano wao na mwenye chombo kwa kuongezwa kihusisho. Kwa hivyo, kihusisho ndicho kinachofanya uhusiano baina ya chombo na mwenye chombo kuwa ni mzuri au mbaya. (Mfasiri).

mbali mbali ya watu, pamoja na mambo tofauti tofauti yaliyotukia katika ardhi hiyo. Jambo hili la kawaida linaeleweka kwa watu wote.

Madola, falme na mataifa yote yanakubaliana kuhusu vitendo hivyo vilivyo kanuni. Kwa sababu ya kuhusika kwa mwenye chombo na chombo, ardhi, majumba na mahali huwa na ubora na uhusiano ambao pia huwekewa kanuni zake.

Ubora huo ndio chanzo cha kuwekwa kanuni zenye itibari ambazo hazipuuziki.

Je, hamuoni kwamba ardhi, viwanja, majumba na maofisi ya kiserikali na hasa yale yanayohusika na mtawala wa nchi huwa na heshima mahususi kuliko vyombo vinginevyo? Je, hamuoni kwamba kuna kanuni maalum zilizowekwa juu ya vyombo hivyo vya kiserikali ambazo kila raia inambidi azifuate?

Vivyo hivyo, ubora na uhusiano huo unapatikana katika ardhi na nyumba zinazohusika na Mwenyezi Mungu ambazo zimewekewa adhana, heshima, sheria, maamrisho na miiko mahususi ambayo kila mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu humpasa kuyaheshimu na kuyafuata.

Kila mwenye kuishi chini ya bendera ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na Uislamu, lazima aheshimu na atekeleze sheria hizo bila ya kipingamizi chochote.

Kwa sababu ya kanuni hiyo ya kawaida yenye kukubaliwa na watu wote imewekwa sheria mahususi kwa ajili ya Kaaba na mipaka yake. Vile vile Msikiti wa Haram (mjim Makka) na Msikiti wa Mtume (mjini Madina) imewekewa sheria mahususi.

Kadhalika, misikiti mingineyo, makanisa, maabadi na mahekalu linamotajwa na kukumbukwa jina la Mwenyezi Mungu yana

sheria zake maalum kuhusu heshima, taadhima, utohara na unajisi na miiko ya kuingia humo kwa mwenye janaba, hedhi na nifasi. Moja katika mambo mahsusi ya maabadi Matakatifu hayo ni kuwa, kwa vyovyote vile hayaruhusiwi kununuliwa au kuuzwa. Walakini, kinyume chake, inaruhusiwa kwa njia kadha, wakati inapoidhinika kuuzwa au kubadilishwa kwa kitu bora zaidi mali ya wakfu ya umma inayowahusu watu.

Kanuni zote zimewekwa kuhusu sehemu hii takatifu kwa sababu ya itibari ya kuhusika kwao na Mwenyezi Mungu, Muumba wa ulimwengu. Kufanywa Makka kuwa mji mtakatifu na wa amani, kuamrishwa watu kwenda kuhiji huko kutoka mahali mbali mbali ili kuzitimitiza ibada za Hija na kuwekwa sheria kuhusu hata mimea na miche ya hapo, inathibitisha kwamba ubora na heshima uliopata mji huo ni kwa sababu ya kuhusika kwake na Mwenyezi Mungu. Hivyo, akaichagua ardhi ya Makka miongoni mwa ardhi zote duniani.

Mji Mtukufu wa Madina pia ni mji wa Mwenyezi Mungu ambao sheria mahususi imewekwa kuhusu wakazi, ardhi na watu wanaozaliwa na kuzikwa humo. Taadhima hii imewekwa kwa sababu ya kuhusika kwa mji huu na Mwenyezi Mungu na kwa kuwa ni mji mkuu na makazi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) wa Mwisho wa Manabii.

Kanuni hii ya kiakili (ya uhusiano wa chombo na mwenye chombo), ingawa haimo katika sheria tukufu mahsusi, inakubaliwa katika Islamu kwa sababu ya mambo yake ya kimaumbile na kidesturi. Kwa kwell, sheria haipambanui ubora kati ya ardhi tofauti, bali maoni ya watu ndiyo yatukuzayo kitu hiki au kile. Ni kanuni ikubaliwaya katika Islamu kwamba tangu Mitume, manabii, mawasii, mawalii, wasadiki, mashahidi na hata jamii ya waaminio, kila mmoja anahitilafiana na mwenzie katika ubora wake.

Asili hii iliyo muhimu sana kwa maisha ya jamii, inaleta umoja, mapenzi na ujamaa. Na hali kadhalika, huleta uadui, chuki na ukorofi inapoongezwa kihusisho kuonyesha uhusiano wa chombo na mwenye chombo.[38]

Mzizi wa mfarakano na uadui ni asili hii hii ambayo huleta umoja, mapatano na amani.

Asili hii ni chanzo cha kuasisiwa kwa vyuo vikuu na vyuo vya mafunzo. Vile vile, uhasama, tofauti na mapigano kati ya mataifa mbalimbali husababishwa na kuhitilafiana juu ya asili hii.

Asili hii ndiyo inayoleta mfarakano wa makabila, vyama na madhehebu.

Kwa asili hii mambo ya kidini, kidunia na kisiasa huendelezwa. Kwayo hufanyika mikutano ya kidini, kielimu, kijamii, kiserikali, kimataifa na kisiasa.

Asili hii husababisha amani na vita, umoja na utengano na ukaribu na umbali.

Ule Utawala wa ulimwengu (chombo) wenye nguvu, mamlaka na madaraka juu ya watu wote ni wa (kihusisho) Mwenyezi Mungu (mwenye chombo), na hakuna mtu yeyote anayeweza kujitoa katika utawala huo.

38 Tuseme kwamba kuna kitabu (chombo) kimoja ambacho hakijulikani kinahusiana na yupi - kama ni cha Mungu au binadamu. Ikiwa kihusiano chombo (kitabu) na Mungu, basi mwenye chombo atakuwa ni Mungu - "Kitabu cha Mungu." Kwa hivyo, inapojulikana ni nani mwenye chombo (baada ya kutumiwa kihusisho), itabidi kila mtu aamini na ayafuate yote yaliyomo katika hicho kitabu cha Mungu. Wale watakaokataa na kupinga kwamba ni Kitabu cha Mungu, watafanya chuki na uadui dhidi ya walioamini. Hivyo, hapa itapatikana hitilafu baina ya makunui mawili kuhusu uhusiano wa chombo (kitabu) na mwenye chombo. Hitilafu hiyo hutokana na kutumika kwa kihusisho 'cha'. (Mfasiri).

Naam, kihusisho hupandisha na huteremsha (vyeo), huunganisha na hutenga, hukaribisha na huubaidisha, huchukua na hutoa, hutukuza na hudhalilisha, hujazi na huadhibu, huadhihisha na hutweza.

Kihusisho humfadhilisha, humtukuza na kumwandimisha askari ambaye alikuwa hajulikani na akawa anasifiwa na kuheshimiwa na serikali na umma hata kwamba anapokufa huwekewa shada la maua juu ya kaburi lake na hukumbukwa milele katika historia. (Kwa sababu alikuwa mkuu wa majeshi ya nchi fulani).

Kihusisho hutuliza na hurahisisha misiba na maafa ya binadamu kwa kumfanya avumilie shida zote. Vile vile humfanya (mtu ajitolee mhanga kwa ajili ya uhusiano huo bila ya kujali mali au roho yake. Kwa sabahu ya kutoa mali na roho yake ili apigane kuokoa dini ya Mwenyezi Mungu).

Kihusisho kilimfanya Mtukufu Mtumc (s.a.w.) abusu maiti ya ahaba wake mtukufu Uthman bin Madh'um huku machozi yakimtiririka mashavuni.[39]

Kihusisho kilimfanya Mtukufu Mtume (s.a.w.) amliliye mwanawe Husain, abusu na anuse udongo wa Karbala, na kila aendapo aukumbuke msiba huo.[40]

---

39 Kitabu kiitwacho *Amaali*, cha Bwana Abul Qasim Abdul Malik Ibne Bushraan; *Musnad*, cha Bwana Abul Hassan Ali Ibne Ja'ad al-Jawhari, Juzuu ya 10; *Mustadrak Sahihain*, Juzuu ya 21

40 Katika kitabu kiitwacho *Musnad* cha Imam Ahmad bin Hambal, Juzuu ya Tatu, Uk. 242 imo Hadithi isemayo:- Sahaba mmoja Bwana Anas bin Malik amesema: "Malaika mmoja wa mvua aliomba ruhusa ya Mwenyezi Mungu kwenda kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.). Mwenyezi Mungu akamruhusu. Mtukufu Mtume (saw.) akamwambia mkewe Umme Salma, 'Angalia mlango, mtu yeyote asiingie,' Umme Salma ameeleza, 'Papo hapo Mtukufu Husain alifika, na alipotaka kuingia ndani, nilimzuia. Husain akachupia na kuingia ndani na kuanza kumpanda Mtukufu Mtume (saw.) mgongoni na shingoni. Malaika akamuuliza (Mtume s.a.w.) "Je, unampenda (mtoto ⇒

(Kwa sababu Imam Husain (a.s.) alikuwa Mpenzi wa Mwenyezi Mungu na Bwana na vijana wa Peponi).

Kihusisho kilimfanya Ummul-Mu'miniyn Bibi Umme Salma aufungefunge udongo wa Karbala katika nguo yake.[40]

Na ndicho kilichomfanya Bibi Fatima (a.s.) binti wa Mtume achukue udongo wa kaburi la Mtukufu baba yake na kuunusa.

Kihusisho kiliwafanya Bani Dhabba waamrishwe kukusanya, kufikicha na kunusa samadi ya ngamia wa Ummul-Mu'numyn Ayesha katika vita vya Jamal. (Kwa sababu Ayesha alikuwa mke wa Mtukufu Mtume s.a.w.).

Kihusisho kilimfanya Amirul-Mu'miniyn Ali (a.s.) alipowasili Karbala achukue fungu la udongo wa Karbala, aunuse na kulia hata ardhi ikalowa kwa machozi yake na huku akisema: "(Siku ya Kiyama) watu sabini elfu watafufuliwa katika ardhi hii na wataingia Peponi bila ya hesabu."[41]

Kihusisho kilimfanya mtu mmoja katika Bani Asad aunuse udongo wa kaburi tukufu la Husain (a.s.) na alie.

⇐ huyu)?" Mtukufu Mtume akajibu, "Ndiyo." Malaika akasema, "Basi ujue kwamba umati wako Watamchinja; na kama unataka nitakuonyesha mahali atakapouawa." Kisha yule Malaika akamuashiria (kwa kidole) na papo hapo akauleta udongo mwekundu. Umme Salma akachukua ule udongo na akaufungafunga katika nguo yake". Hadithi hii imepokewa kutoka kwa Mabwana Muamal-Amara Ibn Zazaan - Thabit - Sahaba Anas bin Malik. Bwana Thabit amesema: "Tulifahamu kwamba ardhi ile ulikotoka udongo huo ilikuwa Karbala." Bwana Sulayman bin Ahmad amesema: "(Kisha) Mtukufu Mtume (s.a.w.) akaunusa udongo ule na kusema, '(Nasikia) harufu ya huzuni na balaa.'" Bwana Sharjiyl bin 'Aun amesema: "Baadaye Mtukufu Mtume (s.a.w.) akaushika mkononi ule udongo alioupewa na Malaika yule na akaanza kuunusa na kulia; na katika hali ya kulia alikuwa akisema, 'Ewe Mola wangu, usimbariki mwenye kumwua mwanangu na mtie motoni'. Baadaye akampa Umme Salma udongo ule."

41 Soma kitabu kiitwacho *Al-Majma*, Juzuu ya Tisa, Uk. 191.

Bwana Hisham bin Muhammad amesema: “Maji yalipopitishwa juu ya kaburi tukufu la Husain na yalipoondoa alama ya kaburi na kudidimia baada ya siku arobaini, bedui mmoja wa kabila la Banu Asad akaja akiwa amechukua fungu la udongo huku akilinusa. Alipofika penye kaburi, akalia na kusema, ‘Nakufidia baba na mama zangu (ewe Husain)! namna gani ulikuwa ukinukia wakati wa uhai wako hata sasa udongo wa kaburi lako unanukia pia!’ Kisha akasoma ubeti huu:

أرادوا ليخفوا قبره عن عداوة

وطيب تراب القبر دل على القبر

“Waliazimia kulificha kaburi lake kwa uadui wao. Lakini harufu nzuri ya udongo wa kaburi iliongoza penye kaburi (hilo).”[42]

Kwa hivyo, kila mwanadamu, awe wa asili, mahali au zamma yoyote, akitaka as1take, mambo yake yote ya maisha yapo chini ya madaraka na mamlaka kama yalivyohusika katika kauli hizi.

(Vihusisho) roho yangu, mwili wangu, mali yangu, watu wangu, mtoto wangu, jamaa zangu, ukoo wangu, biashara yangu, dini yangu, mila yangu, taifa langu, nyumba yangu, nchi yangu na kadha wa kadha (hutumika).[43]

Kwa ujumla ufungano kama huo huingia chini ya madaraka ya serikali, tawala, jumuiya, makabila, mashirika, vyama na kadhalika.[44]

---

42 *Tarikhush-Shaam* cha Bwana Al-Hafidh Ali Hasan Abdul-Qasim ibne Asaakir, Juzuu ya Nne, Uk. 342; *Al-Kifayah* cha Bwana Muhammad Yusuf Al-Kanji, Uk. 293.

43 Kwa mfano: maneno “Nyumba yangu” yanaonyesha kwamba mimi ni mwenye chombo (nyumba) hicho. Ufungano au uhusika huo ndio unaotambulisha ni nani mwenye mamlaka na madaraka juu ya nyumha hiyo. (Mfasiri).

44 Kwa mfano: Kauli, “dini yangu” ina maana kwamba mimi ni mfuasi wa dini fulani, hivyo inanibidi nitii na nitekeleze sheria za dini yangu. (Mfasiri).

Mara tu uhusiano huo unapofungana kwa ujumla au sehemu, moja au wote, basi kwa kawaida, itambidi kila mtu anayehusika afuate na kutekeleza sheria zote zilizowekwa.

Jambo hili muhimu lina faida nyingi ziwezazo kuyatatua matatizo mengi ya kijamii, mathalan, matatizo ya kanuni, itikadi, madhehebu, sheria za kidini, ibada, mambo na vitu vitakatifu vya Kiislamu ambavyo inabidi kuviheshimu na kuvitukuza.

Hapana shaka kwamba maelezo hayo ya kutosha yatabainishia mtafiti wa ukweli siri ya ubora wa udongo mtakatifu wa Karbala na jinsi uhusiano wake na Mwenyezi Mungu Mtukufu ulivyo, na kiwango cha heshima yake (Imamu Husain a.s.) kilivyokaribiana na Mwenyezi Mungu.

Kwa maelezo haya, je una maoni gani juu ya udongo wa Karbala? Udongo ambao ndani yake amelazwa yule kiongozi mkubwa wa "Jeshi la Haki" na ambaye alijitolea mhanga na kuawa kishahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu?

Udongo aliozikiwa Mpenzi wa Mwenyezi Mungu na mwana wa Mpenzi Wake (yaani mwana wa Mtukufu Mtume s.a.w.).

Udongo aliozikiwa yule mtu awaitaye na kuwaongoza watu kwake (yeye Mwenyezi Mungu).

Yule mtu (Imamu Husain a.s.) ambaye alimwaga damu yake kwa ajili ya kueneza neno la Haki, Umoja wa Mungu, kustawisha mafundisho ya dini na kuimarisha njia ya Haki.

Yule Bwana wa Mashahidi ambaye, ingawa ameuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini kwa hakika yu hai anaruzikiwa na Mola wake.[45]

45 Mwenyezi Mungu Anasema, "Wala usidhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu (kuwa) ni wafu; bali ni hai wanaruzukiwa kwa Mola wao (Qur'ani, 3:169).

Yupi katika wafalme na watawala wa dunia, tangu kuimbwa kwa Adamu hadi sasa aliyekuwa na Amiri-jeshi, aliyekuwa mpaji, mnyofu, mkweli, msifika, sharifu na asiye na kifani aliyefidia roho yake kama alivyofidia Imamu Husain (a.s.), aliyekuwa Amiri-jeshi wa Watakatifu wa Karbala?

Kwa nini Mwenyezi Mungu asijivunie kuwa na Amiri-jeshi kama huyo?

Kwa nini Mwenyezi Mungu alizuie japo tone moja la damu kumwagika ardhini wakati Imamu Husam (a.s.) alipotawanya damu yake hewani katika siku ya Ashura?[46]

Kw nini jina lake tukufu lisikumbukwe na kutajwa milele mbinguni na ardhini hali mapenzi ya Mwenyezi Mungu yalikomea katika kiini cha moyo wake?

Kwa nini katika siku ya Ashura ya Husain dunia isiwe giza totoro?

Kwa nini Mwenyezi Mungu asionyeshe alama ya uchungu na ghadhabu yake siku ya kuuawa kwake?

Kwa nini ardhi na mbingu visimlilie (Husain a.s.) kwa majonzi yake? (Tuldo hili limeelezwa na baadhi ya wapokezi wa Hadithi kutoka kwa Ibne Siyrin).

46 Bwana Hasan al-Muthanna amesimulia kutoka kaw Muslim bin Riyah huria wa Imamu Ali (a.s.) kwamba: "Siku ambayo Husein aliuawa kishahidi mimi nilikuwa pamoja naye. Wakati mshale uipomchoma usoni aliniambia, 'Ewe Muslim, kinga damu yangu kwa mikono yako!' Nami nikaikinga mpaka ilipojaa mikononi mwangu, akaniambia, 'Mimina mikononi mwangu!' Nilipommiminia, Mtukufu (Imamu Husain) akanyanyua mikono yake angani huku akisema, 'Ewe Mola wangu, lipiza kisasi cha damu ya mwana wa binti wa Mtume Wako.' (Muslim anaendelea kusema). Hata tone moja katika damu hiyo halikudondoka ardhini." (Soma kitabu kiitwacho *Tarikhush-Shaam* Juzuu 4, Uk. 338 na *Al-Kifayah* Uk. 284). Baadhi ya wapokezi wameeleza hivi: "Wakati mshale ulipomchoma kooni (Imamu) Husain, akarusha damu ya koo lake hewani."

Kwa nini siku hiyo mbingu isinyeshe mvua ya damu?

Kwa nini Mwenyezi Mungu asiwatume malaika wake watukufu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) kumpelekea udongo wa Karbala na ujumbe mahususi?[47]

Na kwa nini Mtukufu Mtume (s.a.w.) asiunuse na kuubusu udongo ule na asiukumbuke maishani mwake mwote? Na kwa nini asiutunze nyumbani mwake kuwa ukumbusho?[47]

---

47 Bwana Abdullah ibne Al-Barqi Misri amenakili (Hadithi moja) kutoka kwa Sahaba mmoja Bwana Abi Salma bin Abdurrahman (isemayo) kwamba (Bwana Abi Salma) amesema: "Ayesha, mke wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikuwa na chumba cha kuwekea vyombo vya chakula. Wakati wowote Mtukufu Mtume (s.a.w.) anapotaka kuzungumza na Jibrail huenda humo. Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w.) alikwenda juu kwenye chumba (hicho) cha kuwekea vyombo vya chakula ili kuonana na Jibrail; na akamwagizia Ayesha kwamba mtu yeyote asijue (kuwa yuko humo). Kwa bahati, chumba cha Ayesha kilikuwepo kwenye ngazi. Husain akaja na akapanda ngazi na akaingia humo chumbani alimo Jibrail kwa haraka hila ya Ayesha kujua.
Jibrail akauliza, 'Huyu ni nani?'
Mtume akajibu, 'Ni mwanangu.'
Hapo Mtume akamkumbatia Husain na kumkalisha pajani mwake. Jibrail akasema, 'Umati wako watamuua'. Kwa kustaajabu, Mtume akasema, 'Umati wangu' Akajibu, 'Ndiyo, na kama unataka nitakuonyesha mahali atatapouawa!!' Kisha Jibrail akafanya ishara (kwa kidole) kuelekea kwenye ardhi ya Taf (iliopo Iraq), mara akatoa udongo mwekundu kutoka huko na akamwonyesha Mtume. Sayyid Mahmoud Madani ameeleza hivi: "Hadithi kama hii imenakiwa na Bwana Ibne Saad isipokuwa mwisho wake imetofautiana kwa maneno haya 'Huu ni udongo wa mahali atakapouawa (Husain)". (Kwa maelezo zaidi soma: *As-Siraatus-Sawiy* cha Sayyid Mahmoud Madani, Uk. 49. Angalia pia vitabu hivi: *Maqtalul Kharazmi* cha Bwana Al-Khatib Al-Hafidh Al-Muwaffak bin Ahmad Kharazmi, Juzuu 1, Uk. 159; *Majma uz Zawad* Juzuu 9, Uk. 187-188; *As-Sawa'iq Muhriqa* cha Allama Ibn Hajar Makki, Uk. 155 na 190; *Khasai-sus-Suyuti* cha Imamu Jalaluddin Suyuti, Juzuu 2, Uk. 125-126; *Kanzul Ummal* cha Bwana Ali Al-Muttaqi Al-Hanafi, Juzuu ya Sita, Uk. 223; *Jawharatul Kalaam*, Uk. 117; *A'laamun Nubuwwat* cha Imamu Abul Hasan Mawardi, Juzuu ya 12, Uk. 83; *Musnad* Ahmad bin Hambal, Juzuu ya 6, Uk. 294; *Majma' ul Kabir* cha Imamu Abul-Qasim Sulaiman bin Ahmad Tabarani n.k.)

Enyi Waislamu halisi! Kwa ajili ya kumkaribia zaidi Mwenyezi Mungu wakati wa kusali sala za mchana na usiku, je, kusujudia udongo kama huo si bora kuliko udongo na ardhi tohara nyinginezo?

Je, si bora zaidi na afadhali kusujudia udongo huo (wa Karbala) kuliko kusujudia zulia au msala (wa kitambaa) ambao haujulikani umesukwa na nani au kwa kitu gani na hali sunna ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) hairuhusu kusujudia zulia au msala (usiosukwa kwa majani)?

Je, kwa ajili ya kumkaribia Mwenyezi Mungu na kuwa mnyenyekevu na mnyonge mbele yake, si bora zaidi na afadhali kwa kiumbe kuweka uso na paji lake juu ya udongo wenye mafunzo ya kumtetea na kupata maarifa ya Mwenyezi Mungu? Udongo ambao ni ushahidi mzuri wa kutetea kanuni ya Mwenyezi Mungu na dini tukufu ya Islamu?

Baada ya kueleweka siri ya kusujudia ardhi, je, haistahiki zaidi kusujudia udongo ambao adhama, utukufu na fahari ya Mwenyezi Mungu vimo ndani yake, na ambao ni mfano bora wa kumwabudu Mwenyezi Mungu na kuonyesha unyenyekevu mbele ya Mola kwa njia iliyokuwa bora kabisa na dhahiri?

Je, si bora na yenye kustahiki zaidi udongo ambao ndani yake mna ushahidi dhahiri wa Umoja wa Mwenyezi Mungu na kujitolea mbele Yake? Udongo ambao huvuta kwenye huruma, mahaba ya moyoni, vema na upole?

Je, si afadhali na bora zaidi kuchagua mahali pa kusujudia pawe juu ya udongo ule uliofoka chemchemi ya damu iiyosharabu rangi ya Pendo la Mwenyezi Mungu na (damu) iliyosimamisha msingi wa sunna yake?

Udongo ambao ulikandwa kwa damu ya (mtu) yule ambaye

Mwenyezi Mungu amemtakasa[48] na kufaradhisha kupendwa kwake kuwa ni malipo ya Utume wa Mtukufu Mtume (s.a.w.)?[49]

Udongo ambao ulikandwa kwa damu ya Bwana wa vijana wa Peponi, Mpenzi wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na amana alioiacha Mtukufu Mtume (s.a.w.) kwa Umati wa Kiislamu?[50]

Kufuatana na misingi hii miwili, sisi Mashia tunatumia vipande vya udongo wa Karbala uliofinyangwa katika umbo la duara au

48 Mwenyezi Mungu Anasema, "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuwekeni mbali na (kila) uchafu, enye watu wa nyumbani (mwa Mtume) (Ahlul-Bait), na kukutakaseni (muwe) tohara kabisa". (Qur'ani, 33:33). Kwa maelezo zaidi kuhusu Aya ya *Tat-hiyr* tazama vitabu hivi: *Sahih Muslim* Juzuu 2, uk. 283; *Musnad* Ahmad Juzuu 1, uk. 330; *Mustadrak-Sahihain* Juzuu 3, uk. 108, 146 na 147. Kufuatana na hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.), Ahlul-Bait (Watu wa Nyumbani mwa Mtume) ambao wametakasika (na ni) tohara kabisa kutokana na kila uchafu na ambao kuwapenda ni lazima, ni Mtukufu Mtume mwenyewe, Ali (binamuye), Fatima (bintiye), Hasan na Husain (wajukuuze) ambao peke yao tu ndio wanaohusika katika aya hii.

49 Mwenyezi Mungu Amesema, "... Sema (ewe Muhammad) kwa hayo (ninayokufundisheni) sitaki malipo yoyote kwenu ila muwe na mapenzi kwa jamaa zangu...". (Qur'ani, 42:23). Kwa maelezo zaidi, kuhusu Aya ya *Mawaddah* tazama vitabu hivi. *Tafsir Al-Kashshaf* cha Bwana Zamakhshari Juzuu ya 2, uk. 339; *Zakhairul 'Ukba* cha Bwana Al-Muhibbuddin At-Tabari, uk. 25; *Matalibus-Su-uul* uk. 8; *Nurul Absar* cha Bwana Shablanji, uk. 112; *Ahyaul Mayyit* cha Allama Hafidh Jalaluddin Sayuti, uk. 239; *Tafsir Tabari* cha Bwana Tabari; *Yanabiul Mawaddah* cha Sheikh Sulaiman Qanduzi.

50 Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema: "Hasan na Husain ni Mabwana wa vijana wa Peponi". (*Jama Tirmidhi* cha Imamu Abu Issa Muhammad bin Isa as-Sulami Tirmidhi uk. 466 na 467; *Sunan Ibne Majah* uk. 12; *Jama Saghiyr* cha Allama Jalaluddin Suyuti, uk. 6).

Vile vile Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema: "Enyi watu! Nakuachieni miongoni mwenu vitu viwili (amana) ambavyo mkivifuata hamtapotea kamwe baada yangu, navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur'an) na Kizazi changu (Ahlul-Bait)". (Soma vitabu hivi: *Sahih Muslim* Juzuu, Uk. 279 na 280; *Jama Saghiyr*, uk. 55; *Jama Tirmidhi*, uk. 467 na 468; *Mustadrak-Sahihain* Juzuu 3, uk. 148 na 533; *Musnad* Ahmad Juzuu 2, uk. 247, Juzuu 3, Uk. 4, 14, 17, 26 na 59, Juzuu 4, uk. 367 na 371, Juzuu 5, Uk. 182)

mraba, ili kusujudia wakati wa kusali; kama alivyokuwa akifanya Masrouq bin al-Adja - mwanachuoni mashuhuri wa Kiislamu ambaye daima alikuwa na kipande cha udongo wa mji wa Madina alichokuwa akisujudia. Bwana huyo a1ikuwa mwanafunzi aliyeelimishwa katika zama za Makhalifa wanne (*Khulafa-ur-Rashidyn*) na alikuwa mwanachuoni mkubwa akiwafundisha watu sheria na sunna za Kiislamu mjini Madina. Kwa hivyo, hayumkiniki kamwe kwamba mtu huyo alikuwa akifanya *bid'a* (jambo lisilo katika sunna za Kiislamu).[51]

Kwa hakika, msingi upi katika hii miwili tuliyoieleza ulio na jambo la kipuuzi au ta kuchukiz.a lisilo la maana?

Msingi upi katika hiyo haufuatani na mwito wa Qur'ani Tukufu au unaopinga sunna za Mwenyezi Mungu na Mtume wake?

Msingi upi katika miwili hiyo usiokuweko tangu zamani au haukutendeka au kujulikana katika zama za Mtume (s.a.w.) hata ukahesabiwa kuwa ni *bid'a*?

Msingi upi katika hiyo haukubaliani na akili au hoja za mwanadamu?

Baada ya kueleza hayo yote, sisi Mashia tunasema kwamba kusujudia udongo wa Karbala si lazima, wala sheria za dini au

51 Ibne Asaakir katika kitabu chake kiitwacho *Tarikhush-Shaam* anaeleza habari ya Abul Hasan Ali Ibne Abbasi hivi: "Abul Hasan aliwaandikia watu wake waliokuwa Makka hivi: "Nileteeni kipande cha jiwe la mlima wa Marwah ili wakati wa kusali nipate kusujudia." Kisa hiki na maelezo hayo yametajwa na Bwana Samhudi katika Kitabu chake kiitwacho *Wafaa-ul-Wafaa* kwamba huyo Abul Hasan Ali Ibne Abdallah Abbasi alikuwa akijulikana sana kwa uchaji na ibada, na ameweka jina zuri miongoni mwa Masunni tanzu zama zake hadi hivi sua. Kwa sababu ya wingi wa elimu yake umezing'arisha kurasa za historia. Kitendo cha mwanachuoni huyo ambaye alikuwa akifuata sunna za Mtukufu Mtume (s.a.w.) hakiwezi kamwe kusemwa kwamba alifanya *bid'aa*.

madhehebu hazikulazimisha; bali kinyume cha dhana ya wale wasioifahamu na kuijua itikadi ya Shia, hakuna Shia hata mmoja hadi hivi sasa ambaye hustahabu zaidi kusujudia udongo wa Karbala kuliko udongo mwingine isipokuwa tu kwamba kufuatana na akili na hoja, udongo wa Karbala unastahiki zaidi kusujudiwa, kama tulivyoeleza hapo awali.

Wanavyuoni wengi wa Kiislamu katika safari zao walikuwa wakichukua kitu kingine kinachoruhusiwa kusujudia (kisichokuwa udongo wa Karbala) kama vile mkeka au msala uliosukwa kwa majani baada ya kuhakikisha utohara wake.

Kwa kuzingatia, kuheshimu na kutukuza hii msingi miwili madhubuti na kwa kufuatana na maoni yetu juu ya wakazi na waliohamia miji miwili mitukufu ya Makka na Madina, ni lazima kwao kutumia udongo wa sehemu mbili hizo kwa ajili ya kusujudia. Kwa kufanya hivyo, kwa upande mmoja atakuwa ameifuata misingi hii muhimu na kwa upande mmoja atakuwa ameifuata mii hu muhimu, na kwa upande wa pili, watajilinda kutokana na joto kali la ardhi ya misikiti hiyo wakati wa adhuhuri. Vile vile wataweza kusujudia udongo ulio tohara na mtakatifu wanapokuwa kwao au safarini; na kwa kufanya hivyo watakuwa wameufuata mwenendo wa mababu wachamungu, kama vile wanavyuoni mashuhuri Bwana Abul-Hasan Ali bin Abdalla Abbasi na Bwana Masrouq bin Al-Adja, ambao visa vyao tumekwishavitaja.

Baada ya kueleza umuhimu wa udongo, inabidi pia viwekwe vipande vya udongo mahali ambapo mahujaji na wenye kuzuru maziara matakatifu hufika, ili umma wa Kiislamu uweze kuwa navyo na kuvichukua makwao na kuwa ukumbusho, kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kila Muislamu akiuangalia udongo atakumbuka na kupata harufu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na Unabii wa Mtume wake (s.a.w.). Na vipande hivyo vya udongo vitakuwa kama taa zitoazo nuru katika majumba ya

Waislamu na kutia nuru nyoyo zao. Na Waislamu popote wawapo watakaposujudia udongo ule wataweza kumkaribia zaidi Mwenyezi Mungu; kwani ni udongo unaotoka katika ardhi bora kabisa ambayo Mwenyezi Mungu ameifanya kwa ajili yake, kuwa ni makao makuu ya amani, usalama na Jumba Kuu lake (Kaaba), na kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) ameifanya kuwa ni maskani na malazi yake Matukufu.

Katika ardhi hizi mbili za sehemu takatifu, kuna wito wenye nguvu kwa ulimwengu wenye kuongoza kwenye Uislamu, ibada ya Kaaba na mji mkuu wa Mtume (s.a.w.) na sunna zake.

Mwenyezi Mungu anasema, "... Na anayeviheshimu vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu, basi hiyo ni kheri kwake na mbele ya Mola wake ...." (Qur'ani, 22:30).

TAMATI

ISBN: 9976 956 52 5



Kimetolewa na Kuchapishwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P 20033
Dar es Salaam